**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

"Kotra" Nyerere Road,
S.L.P. 377,
MUSOMA,
Barua Pepe: rbcmara@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**
www.pccb.go.tz

**MUSOMA, MARA – MEI, 2022**

# CHAMBUZI ZA MIFUMO ZABAINI VIASHIRIA VYA RUSHWA MKOANI MARA

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa mara nyingine tena ninawakaribisha sana katika ofisi za **TAKUKURU** Mkoa wa Mara. Shukrani za pekee zimwendee Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuifikia siku hii ya leo. Lengo kuu la kukutana kwetu ni kutoa taarifa ya utendaji kazi wa ofisi yetu ya TAKUKURU Mkoa wa Mara kwa kipindi cha miezi mitatu ambayo ni kuanzia Januari hadi Machi, 2022.

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi hicho cha Januari – Machi, 2022, **TAKUKURU** Mkoa wa Mara imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 kama ifuatavyo:-

## ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022, katika kutekeleza jukumu lake la kuelemisha na kushirikisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Mara imefanya mikutano ya hadhara 45 na semina 49 katika Wilaya zake za Bunda, Rorya, Serengeti, Butiama,Tarime na Musoma, lengo likiwa ni kuwaelimisha wananchi kuhusu wajibu wao wa kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya Rushwa.

Pia tumefanya vipindi vitatu (3) vya Redio, kuimarisha klabu 90 za wapinga rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo na kufanya maonesho 4.

Aidha, katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Mara iliweza kuutambulisha kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Mwongozo wa Mafunzo kwa Wawezeshaji wa Kufundishia Vijana wa Skauti Kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Mwongozo huu umekabidhiwa kwa Wakuu wa Wilaya kwa kuwa wao ndiyo Walezi wa Skauti katika Wilaya zao. Lengo kufanya hivyo likiwa ni kuwajenga vijana katika misingi ya Uzalendo, Uwajibikaji na kutojihusisha na Vitendo vya Rushwa.

Vile vile tumefanya Mikutano na wananchi kwa kuwashirikisha watumishi wa Idara zingine za Serikali kupitia programu inayojulikana kama TAKUKURU inayotembea kama ifuatayo;

- Tarehe 12/2/2022 katika Kijiji cha Motukeri kata ya Natta, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kulifanyika Mkutano wa Hadhara ambapo TAKUKURU, Kamati ya Usalama Wilaya pamoja na Watumishi wa Idara ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Vijijini (RUWASA) walisikiliza kero za wananchi na majibu yakapatikana papo kwa papo
- Tarehe 28/2/2022 katika Mnada wa Ochuna kata ya Nyathorogo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kulifanyika Mkutano wa pamoja wajumbe wakiwa ni Watumishi wa TAKUKURU, Idara ya Mipango na wananchi ambapo kero kubwa toka kwa wananchi hao ilikuwa ni kwa Wafanya biashara kupunguza ujazo wa chombo cha kupimia Mahindi kinachojulikana kwa jina la 'Kasuku' jambo ambalo linaonekana kuwa ni wizi. Majibu yalipatikana hapo kwamba ukaguzi ufanyike kila mara ili kudhibiti wizi huu.
- Tarehe 11/3/2022 katika kijiji cha Bungurere Kata ya Muriba Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, TAKUKURU kwa kushirikiana na na Watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Victoria, Afisa Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Afisa Misitu na Wananchi wa Kijiji hicho walifanya kikao cha pamoja juu ya utatuzi wa mgogoro wa Chanzo cha Maji Biriri. Wananchi walikuwa na malalamiko ya kuonewa na Kamati ya Mazingira ya Kijiji kwa kupiga hatua za kuruka na kufanya maeneo yao kuwa sehemu ya Hifadhi ya chanzo cha maji. Utatuzi wa mgogoro huu ulipatikana.

- Mnamo tarehe 23/3/2022 TAKUKURU kwa kushirikiana na Jeshi la Zima moto na Uokoaji Mkoa wa Mara, Idara za Biashara, Uandisi na Ujenzi Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Ofisi ya TANESCO Musoma na watumishi wa Idara mbalimbali katika Kata ya Nyasho tulifika katika Soko la Wauza Mitumba eneo la Nyasho Musoma Mjini na kuzungumza na Wafanya Biashara wa Soko hilo. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kusikiliza kero zao mbalimbali na kuwapatia utaratibu juu ya namna ya kujipanga na hatari ya mlipuko wa moto ikizingatiwa kuwa njia za kupita gari la zima moto zimezibwa na baadhi ya wafanya biashara hao. Ilisemekana kuwa Mtendaji wa Kata hiyo anayejitambulisha kama raisi wa kata ana watu aliowapatia maeneo ya biashara kinyemela na kwamba wao ndio wameziba njia hizo za tahadhari. Ilihamuliwa kuwa ndani ya siku 14 njia zote zibaki wazi.
- Mtakumbuka vile vile kuwa kuanzia tarehe 23/1/2022 hadi 1/2/2022 kulikuwa na Wiki ya Sheria Kitaifa ambapo Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Wadau wake ilikuwa ikitoa elimu juu ya sheria mbalimbali kwa makundi mbalimbali ya wananchi, TAKUKURU Mkoa wa Mara ilishiriki katika wiki hii ya elimu kwa kutoa mada mbalimbali kupitia Redio, semina na kwa njia ya kuwa na Mabanda ya Maonesho katika maeneo mbalimbali ndani ya mkoa wetu.
- Tarehe 8-3-2022 katika Viwanja vya Mwenge ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama tulishiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake yaliyofanyika ki Mkoa ambapo tulitoa mada juu ya "Athari za Rushwa ya Ngono" kwa wananchi zaidi ya mia nane wengi wao wakiwa ni akina mama. Zoezi hili liliambatana na maonesho ambapo tulikuwa na banda mahali hapo kwa ajili ya uelimishaji zaidi wa umma.

**UZUIAJI RUSHWA**

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mara imefanya kazi ya ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo 415,** yenye jumla ya **shilingi Billioni 19.1 (sh**. **19,194,779,723.20)** katika Sekta za Elimu, Afya, Maji na Barabara.

Miradi hiyo ni pamoja na ile inayotekelezwa na fedha za Tozo ya Mafuta, Tozo ya Simu, Mfuko wa Jimbo, mapato ya ndani na Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19.

Lengo la ufuatiliaji huu ni kuangalia iwapo kuna mianya ya Rushwa kwenye utekelezaji wa miradi na kuongeza uwazi na upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye miradi ya Serikali ili kuboresha huduma kwenye shughuli za Serikali.

Mapungufu machache yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi hii ni pamoja na upatikanaji wa mafundi ujenzi bila kufuata utaratibu; ununuzi wa vifaa vya ujenzi visivyolingana na idadi inayotakiwa na Kamati ya Manunuzi kuwa ya mtu moja. Mapungufu haya ambayo yangeachwa yangeweza kusababisha mianya ya rushwa, yalifanyiwa kazi kwa kufanya vikao na wadau wa miradi husika pamoja na kuwapa elimu kwa lengo la kuondoa mianya ya rushwa. Elimu hii pia itasaidia katika kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kusisitiza uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma ili kupata miradi bora yenye kukidhi thamani ya fedha (Value for money).

## UCHAMBUZI WA MIFUMO

### Ndugu Wanahabari,

TAKUKURU mkoa wa Mara, imefanya Uchambuzi wa mfumo katika Sekta mbalimbali kama ifuatayo;

1. Sekta ya Sheria kuhusu Mfumo wa upatikanaji wa dhamana Polisi:

2. Sekta ya Afya kuhusu Ukusanyaji wa Tozo ya huduma katika Kituo cha Afya Nyasho:

3. Sekta ya Madini kuhusu Mfumo wa ukusanyaji wa tozo ya huduma katika soko la madini Musoma:

4. Sekta ya Usafirishaji kuhusu Mfumo wa utendaji kazi wa Wakala wa Ufundi na Umeme - TEMESA Mkoa wa Mara.

5. Sekta ya Elimu kuhusu Mfumo wa utoaji wa taarifa za mahitaji ya miundombinu ya Elimu, hususan vyumba vya madarasa na madawati.

6. Sekta ya fedha, kuhusu Mfumo wa usimamizi wa mapato yanayotokana na ushuru wa madini ya ujenzi wilayani Rorya:

Baada ya uchambuzi huo, mapungufu machache ya kiutendaji yaliyobainika yalijadiliwa katika Warsha na wadau wa mamlaka husika, na kukubaliana mikakati ya namna bora ya kuondoa changamoto hizo.

## UCHUNGUZI

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022 jumla ya malalamiko **139** yalipokelewa, kati ya hayo malalamiko **106** yalihusu vitendo vya rushwa na malalamiko **33** hayakuhusisha vitendo vya Rushwa. Kutokana na malalamiko **33** ambayo hayakuhusu rushwa, walalamikaji walihitaji ufafanuzi zaidi na walielemishwa, kushauriwa na kuridhika. Malalamiko **106** yanayohusu rushwa yamefunguliwa majalada ya uchunguzi na yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kukusanya nyaraka za ushahidi pamoja na kuwahoji mashahidi na watuhumiwa.

Katika kipindi hicho uchunguzi wa **majalada manne (4)** ulikamilika, **kesi 6 mpya** zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi zinazoendelea Mahakamani mpaka sasa kuwa **20**.

Kesi **2** ziliamuliwa Mahakamani ambapo kesi 1 mshitakiwa alipatikana na hatia na kesi 1 mshitakiwa aliachiwa huru.

Mchanganuo wa malalamiko **139** yaliyopokelewa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo-:

| SN | IDARA/SEKTA | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | Ushirika | 2 |
| 2 | Binafsi | 3 |
| 3 | Polisi | 6 |
| 4 | Elimu | 14 |
| 5 | Mahakama | 15 |
| 6 | TAMISEMI | 58 |
| 7 | TANAPA | 1 |
| 8 | Afya | 12 |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Kilimo | 1 |
| 10 | Bima | 1 |
| 11 | Ardhi | 13 |
| 12 | Maji | 2 |
| 13 | Fedha | 6 |
| 14 | Dini | 1 |
| 15 | TANESCO | 3 |
| 16 | Madini | 1 |
| | **JUMLA** | 139 |

**MIKAKATI KWA KIPINDI CHA APRILI– JUNI, 2022**

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha Aprili – Juni, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mara tunatarajia kuongeza nguvu zaidi kwenye **KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA** kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji habari ili kubaini vitendo vya rushwa kabla havijafanyika na pia kuchukuwa hatua kali za kisheria kwa wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa

Vilevile, kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mara itafanya uelimishaji wa jamii hususan kupitia ushirikiano kati ya TAKUKURU na Chama cha Skauti nchini kupitia Mpango unaojulikana kama TAKUSKA unaolenga kuwafikia vijana wengi zaidi katika mkoa wetu.

**WITO:**

**Ndugu Wanahabari,**

Mwisho natoa shukurani kwenu Wanahabari kwa ushirikiano wenu mkubwa katika Mapambano dhidi ya Rushwa. Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Mara inatoa wito kwa jamii ya wana-Mara kwa ujumla kutokujihusisha na vitendo kuomba na kupokea rushwa.

Hivyo tunatoa rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mara kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 au kupiga simu ya Mkuu wa

TAKUKURU Mkoa ambayo ni **0738-150130** au kufika katika ofisi za TAKUKURU iliyo karibu nawe.

Pia bado kumeendelea kuwepo na wimbi la matapeli wanaojifanya ni maafisa wa TAKUKURU ambao hupiga simu kwa watu mbalimbali wakitoa maelekezo na maagizo kwa watu hao ikiwa ni pamoja na kutakiwa kuripoti ofisi fulani ya TAKUKURU au kutaka kuonana na wahusika.

Tunatoa wito na rai kwa jamii na watumishi wote ambao ikitokea wamepigiwa simu na matapeli hao basi wajiridhishe na ofisi ya TAKUKURU iliyoko karibu na maeneo yao au kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 na simu rasmi za TAKUKURU Mkoa wa Mara ambayo imetajwa hapo juu. Usikubali kutapeliwa, toa taarifa TAKUKURU ili mhalifu huyo aweze kuchukuliwa hatua za kisheria kwani ni kosa la jinai kujifanya Afisa wa TAKUKURU.

Kwa pamoja tushirikiane kuitokomeza rushwa

***TANZANIA BILA RUSHWA INAWEZEKANA NA KAZI IENDELEE***

**Imetolewa na:**

**Hassan Mossi**
**Mkuu wa TAKUKURU (M) Mara**
**Simu: 0738150130**